TANGAZO LA SERIKALI NA. 533 la tarehe 28/6/2024

SHERIA YA USHURU WA BIDHAA,
(SURA YA 147)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 128)*

AMRI YA MSAMAHA WA USHURU WA BIDHAA KWENYE GARI MOJA LINALOINGIZWA NCHINI NA ABBOTT FUND TANZANIA KWA AJILI YA MATUMIZI YA KIOFISI NA UFUATILIAJI WA MIRADI YA MWAKA 2024

Jina na kuanza kutumika

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Ushuru wa Bidhaa kwenye Gari Moja Linaloingizwa Nchini na Abbott Fund Tanzania kwa Ajili ya Matumizi ya Kiofisi na Ufuatiliji wa Miradi ya Mwaka 2024 na itachukuliwa kuwa imeanza kutumika tarehe 21 Mei, 2024.

Msamaha

2. Kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika aya ya 3 na masharti mengine yoyote kama yatakavyoainishwa na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, ushuru wa bidhaa unaopaswa kulipwa kwa gari lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii lililoingizwa au kununuliwa nchini kabla ya kibali kupitia forodha na Abbott Fund Tanzania kwa ajili ya matumizi ya ofisi na ufuatiliaji wa miradi yake unasamehewa.

Masharti

3. Msamaha uliotolewa chini ya Amri hii utakoma na ushuru wa bidhaa utapaswa kulipwa kana kwamba msamaha chini ya Amri hii haujatolewa ikiwa gari tajwa litatumika kwa matumizi mengine au kuhamishwa au kuuzwa kwa mtu mwingine ambaye hastahili kupata manufaa yanayotolewa na Amri hii.

Ukomo

4. Amri hii itakoma kutumika tarehe 17 Septemba, 2024.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| Na | Maelezo | Namba ya Chesesi | Namba ya Injini |
|---|---|---|---|
| 1 | TOYOTA LANDCRUISER STATION WAGON | JTMAACBJ80-4070864 | F33A-0076056 |

Dodoma,
19 Juni, 2024.

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU,
*Waziri wa Fedha*